



Walitimiza mahitaji yao
kutokana na juhudi zao. Eba
alitaka wanawe wastarehe.
Hawakufanya kazi zozote.



Baada ya muda, Lelisa
alifariki.



Hata baada ya kifo cha
mkewe, Eba hakutaka
wanawe wamsaidie.
Alizifanya kazi zote za
shambani na za nyumbani.



Muda ulipopita, Eba alizeeka na kudhoofika. Alihofia maisha ya wanawe. Alijiuliza, "Wanangu wataishi namna gani nitakapofariki?" Alijua kuwa hawangeweza kujitegemea.



Eba aliwaita wanawe akawaambia, "Urithi mtakaopata kutoka kwangu ni dhahabu nyingi iliyofichwa shambani. Ni juu yenu kuyalima mashamba ili muipate dhahabu hiyo."



Eba pia aliwaambia majirani,
"Nadhani niko karibu
kufariki. Wanangu hawajui
kujitegemea. Nawasihi
mwasaidie hadi
watakapoweza kujikimu
wenyewe."



Baada ya Eba kufariki,
majirani waliwapa wanawe
chakula kwa muda.



Ndugu hao hawakutaka
kuporwa dhahabu
iliyofichwa na baba yao.
Waliamua kuyalima
mashamba wenyewe ili
waipate dhahabu hiyo.



Waliyalima mashamba moja
baada ya jingine. Ila
hawakupata dhahabu
yoyote.



Mmoja alimwuliza mwingine, "Je, unadhani baba alitudanganya?" Yule akajibu, "La, ninadhani baba aliquwa na maana kuwa ukulima ni dhahabu."



Kwa hivyo, kama wakulima
wengine, wana hao
waliyalima mashamba yao.
Walipanda mimea wakawa
matajiri sana.

